SautiElimu

hakielimu

Toleo la 10
2005

ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org



Mwananchi: Hii ni nchi yako!

Rakesh Rajani, Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Mwananchi ni nani?
Ni wewe. Ni mimi. Ni familia na jamaa. Jirani. Rafiki. Ni sisi sote.

Nchi hii ni ya nani?
Ni nchi yetu. Kwa sababu mimi ni mwananchi. Na wewe ni *mwana-nchi.* Sisi sote ni *wana-nchi*. Wazee. Wadogo. Wanawake. Wanaume. Matajiri. Wanyonge. Wote.

Hata ikiwa nchi ni nzuri au mbaya, inatenda haki au haitendi kabisa, inategemea kwa kiasi kikubwa ni nini tunafanya. Inategemea tunavyofikiri na tunavyochukua hatua.

Mara nyingi watu wanaongea kana kwamba nchi yetu ni mali ya viongozi tu, au wakubwa- *'wenye-nchi'*- na kazi ya mtu wa kawaida ni kupokea anachopewa na kufuata amri. Lakini hii si kweli. Kuwa mwananchi anayewajibika ni kujenga demokrasia na kuleta maendeleo kila siku, tukianza na mimi na wewe. Halafu, kama alivyosema Mwalimu Nyerere, hata viongozi watafuata.

Nakala hii ya *SautiElimu* ina mifano mingi ya *wana-nchi* wanavyochangia demokrasia na maendeleo kila siku. Mathias Ndeki wa Mwanza anasema tusisubiri amri kabla ya kuchukua hatua, na anatoa mifano hai. Ayoub Mkumbuki wa Tanga anaeleza namna viongozi wa vijiji wanavyotakiwa kutowakatisha tamaa wananchi walio katika kamati za shule.

Waandishi wetu pia wanatukumbusha kuwa si sawa kuridhika na mafanikio ya baadhi ya watu kama wengine wanaendelea kuachwa pembeni. Mwendo Mnamba wa Mtwara anaeleza wazi jinsi watoto kutoka familia maskini wanavyokosa elimu ya sekondari. Hivi karibuni Bungeni, Serikali imekiri kwamba suala la elimu ya msingi kwa walemavu halijafanyiwa kazi vya kutosha, na haki inahitajika ili kuleta mabadiliko ya haraka. Hata hivyo, katika makala yake James Mikenze anatuambia namna Biseko Busanya, mwanafunzi mwenye ulemavu Ukerewe anavyotia 'fora'.
Hongera Biseko!

Na wewe je? Ni nchi yako. Anza leo. Ifanye iwe nchi ya kufurahia.

Tusisubiri amri, tulete mabadiliko

Mathias Leonard Ndeki, SLP 10252, Mwanza

Nasifu na kupongeza jitihada za taasisi mbalimbali katika kuboresha elimu nchini. Jamii imeanza kujitambua na kuelewa mambo yanayohusu upatikanaji wa elimu, umuhimu wake na hata kuwawajibisha viongozi ambao wanasimamia elimu katika maeneo yao.

Awali katika maeneo mengi hasa vijijini watoto wa kiume ndio waliopewa elimu. Wasichana hawakupata nafasi, labda katika familia zenye upeo wa elimu. Inatia moyo kuona jinsi ambavyo familia nyingi katika maeneo yetu zimeanza kuwaandikisha na kufuatilia mahudhurio ya watoto wao wa kike shuleni. Hayo ni mafanikio japokuwa kuna maeneo ambayo bado yako nyuma.

Yapo matatizo ambayo tunaweza kuyashughulikia kama jamii bila kusubiri amri za viongozi kutoka juu. Mfano, kudhibiti utoro wa watoto wetu, kupambana na tatizo la mimba kwa watoto wa kike na kutokuwaajiri watoto ili wapate fursa ya kupata elimu. Mengine ni kuacha ubaguzi wa kijinsia katika kuwapa watoto elimu. Tusiishie kuwapa elimu ya msingi tu, wanastahili elimu ya juu pia.

Kasi ya maendeleo itaongozeka endapo jamii itashiriki kuboresha elimu kwa vitendo. Uzoefu unaonyesha kuwa maendeleo katika maeneo mengi yamepatikana kutokana na jitihada za jamii yenyewe kufuatilia na kutatua kero zao. Jitihada za wananchi zinawawezesha kupanga mahitaji, kusimamia miradi yao na hata kuchagua na kuwawajibisha viongozi pamoja na taasisi mbalimbali zinazofanya kazi katika maeneo wanayoishi.

Iwapo wananchi watajitolea na kushiriki kikamilifu katika kupanga na kusimamia maendeleo yao wanaweza kuleta mabadiliko makubwa!

Undeni vikundi kufuatilia utekelezaji

Mkereketwa wa Maendeleo, SLP 12630, Dar es Salaam

Mara nyingi watanzania tumeshuhudia viongozi wetu wakitoa maagizo kuhimiza uongozi bora na uwajibikaji katika kuleta maendeleo ya nchi.

Mfano wa kauli zinazotolewa ni kama vile, 'Maafisa wa serikali lazima wawajibike ili kuhakikisha fedha za shule zinapelekwa kwa wakati unaofaa.'

Hakika kauli hizo zinaleta matumaini kwamba kweli Serikali imepania kuboresha elimu kwa kuzingatia maadili ya uongozi bora.

Kinachoshangaza ni kuona baada ya kauli kama hizo hakuna ufuatiliaji wowote. Inakuwa kama mchezo wa kuigiza ambao ukiisha, unaachwa kwa watazamaji na wasikilizaji kufikiria na kuamua hatma yake.

Ushauri wangu kwa viongozi wetu ni kufuatilia utekelezaji wa kauli wanazotoa. Kwa mfano, ikiwa agizo ni 'Kila kiongozi wa wilaya awajibike kusimamia miradi ya elimu' basi ni vyema kuonyesha ni vipi hao viongozi wanatekeleza agizo hilo.

Mathalan kufahamu kama je, wanatoa taarifa za mwezi kwenye mikutano ya wananchi na vikao vya wilaya husika? Je wanawasilisha muhtasari wa utekelezaji wa maagizo kwa wizara husika? Kwa wananchi je?

Nashauri wananchi katika maeneo yao waunde vikundi au kamati za kufuatilia utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na viongozi. Maagizo yasiyokuwa na ufuatiliaji ni vyema yasitolewe kwani yanasababisha wananchi kukosa imani na Serikali.

Demokrasia, utawala bora vianzie shuleni

Juma Kalwani, SLP 186, Mugumu-Serengeti

Wanafunzi wakiwa shuleni hujifunza mambo mengi. Matendo ambayo huyaona yakifanywa na walimu dhidi yao au baina ya walimu wenyewe huyachukulia kama mwongozo wa kuendesha maisha yao.

Walimu wafahamu kuwa kazi yao haiko upande wa taaluma pekee bali pia kuwajenga watoto katika maadili bora.

Baadhi ya walimu wamekuwa wakipandikiza fikra mbaya kwa watoto bila wao kujua. Mfano, mwalimu mkuu anapomfokea mwalimu mwingine mbele ya wanafunzi inajenga dhana kwamba aliye madarakani anapaswa kuwakandamiza walio chini yake.

Wakati mwingine utakuta watoto wa walimu au watoto wanaotoka kwenye familia zenye uwezo wanapewa upendeleo katika mambo mbalimbali kama uongozi shuleni.

Hapa watoto wanajifunza nini? Labda kuwa thamani ya mtu na umuhimu wake vinatokana na uwezo ama madaraka aliyo nayo.

Kazi ya kujenga demokrasia na utawala bora ianzie shuleni ili watoto wakue na mawazo hayo na baadae watimize wajibu na majukumu yao kwa uwazi na uwajibikaji wakizingatia haki, utu na usawa.

Walimu ndio msingi wa taifa lenye kuzingatia maadili ya uongozi bora. Hivyo basi wawe makini wanapotekeleza majukumu yao shuleni. Hadhi ya jamii na taifa linategemea jinsi walimu watakavyowaandaa wanafunzi.



Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 10
2005
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Jamii isiachie siasa kuathiri ushiriki wa wananchi

Ayoub Mkumbuki, SLP 1032, Tanga

Huku kwetu kumetokea mgongano wa maamuzi kati ya kamati ya shule na uongozi wa kijiji. Mgongano huo umesababishwa na tofauti za kiitikadi.

Mathalan, utakuta kamati imeazimia kutekeleza mipango fulani ya maendeleo na inahitaji msaada wa uongozi wa kijiji na wananchi. Uongozi wa kijiji hukataa hata kuwapa taarifa wanakijiji kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mipango iliyopitishwa na kamati ya shule.

Kutokana na tofauti zao kiitikadi, uongozi wa kijiji unahofia kwamba kwa kuhimiza wananchi kushiriki utaipa kamati ya shule umaarufu wa kisiasa. Matokeo yake shughuli za maendeleo ya shule zimekuwa zikikosa mchango wa wazazi na jamii. Wananchi wamekuwa na hofu kwamba wakishiriki wataonekana kuwa wameegemea upande wa chama fulani.

Upo umuhimu wa kuwa na demokrasia ya vyama vingi nchini lakini wananchi wasiruhusu itikadi kuyumbisha maendeleo yao. Jamii isiwaruhusu viongozi wenye itikadi kali za kisiasa kukwamisha maendeleo katika huduma mbalimbali za jamii.

Siasa itumike kuibua mijadala na kutoa changamoto ili kuleta maendeleo. Hatutafika popote endapo tutaelekeza nguvu zetu kwenye mabishano ya kisiasa badala ya kuchangia maendeleo.



Mtoto mwenye ulemavu atia fora Ukerewe

James Mikenze, HakiElimu-Ukerewe

Biseko Busanya ni mtoto anayesoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Musozi wilayani Ukerewe. Busanya, ambaye ni mlemavu wa viungo, alikuwa na mahudhurio mazuri shuleni kuliko wanafunzi wote kwa mwaka 2002 na 2004.

Kutokana na jitihada zake, Chama cha Walemavu (CHAWATA) wilayani Ukerewe kwa kushirikiana na jamii walimzawadia baiskeli (Tricycle) ili kumwezesha kufika shuleni bila kuchoka. Sasa Busanya anaenda shuleni bila adha ya kutambaa kwenye tope na vumbi kama ilivyokuwa awali. Kupata baiskeli hiyo kumemwongezea ari ya kupenda shule.

Mfano huo unatuonyesha kuwa watoto wenye ulemavu wana uwezo na wanapenda kupata elimu kama wengine. Wanachohitaji kutoka kwa jamii ni kupewa fursa na vifaa. Kuwapa elimu watoto wenye ulemavu ni kuwawezesha kumudu maisha yao bila kuwa tegemezi kwa familia na jamii.

Kuna wazazi na walezi ambao bado wanawaficha watoto wenye ulemavu na hivyo kuwatenga na jamii na kuwakosesha elimu. Ni muhimu kwa wazazi, kamati za shule, serikali za mitaa na vijiji, kata na vikundi vya jamii kuhakikisha kuwa watoto hao wanapata elimu.

Tufuatilie kuona je, wanaandikishwa shuleni? Wanafikaje na wanahudhuria masomo? Wanapata vifaa kulingana na mahitaji yao? Mazingira ya shule mfano vyoo na madarasa vinakidhi mahitaji yao? Watu wenye ulemavu wakipata vifaa na mazingira bora wana uwezo wa kufanya mambo sawa au hata kuwazidi wasio na

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukrani kwa *Marafiki wa Elimu* Songea na Faraja Kihongole wa DTV/Channel ten kwa picha.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani

Timu ya *SautiElimu:*
Lilian R. Kallaghe na Nyanda Shuli

Tuandikie!

HakiElimu, ***SautiElimu***
S.L.P. 79401
Dar es Salaam
Simu: (022) 2151852 au 3
Faksi: (022) 2152449
Baruapepe: media@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821 5076

© HakiElimu, 2005



Barua kwa SautiElimu

Adhabu hizi zinaathiri elimu

Shabani Wambali, SLP 898, Ujiji-Kigoma



Shule ni mahali ambapo wanafunzi wanaenda kujifunza. Si sehemu ambapo wakosaji wanaadhibiwa na kudhalilishwa. Kwa mtazamo huo, sioni umuhimu wa kutoa adhabu kali shuleni. Kukosea ni jambo la kawaida katika kujifunza. Mtoto anapokosea haina maana kuwa hafundishiki.

Baadhi ya walimu wanatoa adhabu kali kwa wanafunzi kwa makosa madogo madogo kama kuchelewa shuleni. Pengine wangefuatilia kujua vikwazo vilivyosababisha baadhi ya wanafunzi kuchelewa, wasingetoa adhabu kali.

Hali kama hii inawaathiri wanafunzi kisaikolojia. Wengine wanafikia hatua ya kuwaogopa walimu pindi wanapowaona wakiingia darasani kufundisha.

Katika baadhi ya shule utakuta wanafunzi wanafanya adhabu huku wenzao wakiendelea na masomo darasani. Hivi hakuna namna nyingine ya kuwaadhibu wanafunzi bila kuwakosesha masomo?

Kutokana na kukosa vipindi wengine wamefeli masomo. Walimu ni walezi, watoapo adhabu iwe ni ya kumsadia mwanafunzi kujifunza na si vinginevyo.

Usawa na haki za binadamu nguzo katika elimu

Danford Mlagala, Shule ya Sekondari Chala, SLP 15, Sumbawanga

Tukitaka mafanikio ya kweli ni lazima tuboreshe elimu katika ngazi zote. Hatuwezi kufanikiwa katika hili iwapo hatutajali usawa, haki za binadamu, kuheshimiana, kuthamini utu na kushirikiana miongoni mwa wanafunzi, wazazi na walimu katika shule zetu.

Serikali iweke mkazo katika elimu kwa kuwahimiza watendaji wake kusimamia vizuri mipango ya maendeleo kwa kuzingatia mbinu shirikishi na kuheshimu haki za binadamu. Ikiwa watendaji wa elimu watafanya kazi kwa kushirikiana na wananchi watasaidia kuchochea mafanikio katika elimu. Ushiriki unaweza kuwa wa kusikiliza na kuthamini maoni ya wananchi na kuwapa taarifa mbalimbali zinazohusu maendeleo yao.

Watendaji wa Serikali watumikie jamii bila kubagua jinsia, rangi, utajiri, dini, kabila na hata maumbile. Kwa mujibu wa katiba ya nchi, binadamu wote ni sawa hivyo wana haki na fursa sawa katika kupata huduma mbalimbali za jamii.

Watoto familia duni wakosa elimu ya sekondari

Mwendo Mnamba, SLP 479, Mtwara

Pamoja na kuwepo maendeleo katika sekta ya elimu hapa nchini bado familia duni zinakumbwa na vikwazo katika kuwapa elimu watoto wao.

Tatizo kubwa kwa sasa ni uhaba wa shule za sekondari. Shule hizo bado ni chache ukilingisha na wahitimu wanaomaliza masomo ya elimu ya msingi. Tumeshuhudia kundi kubwa la wanafunzi waliofaulu shule za msingi mwaka jana wakikosa nafasi kuendelea na elimu ya sekondari.

Watoto wanaotoka familia duni ndio wanoathirika zaidi. Hawana uwezo wa kujiunga na shule binafsi ambazo zinatoza ada kubwa ukilinganisha na shule za serikali.

Ninaiomba serikali isimamie vizuri pesa ilizokopa ambazo tutadaiwa ili kuleta mabadiliko katika elimu ya sekondari.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ukisimamiwa vizuri utatufikisha mbali.

Mapungufu na changamoto zilizojitokeza katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) vituongoze kuboresha utekelezaji wa MMES.

Nawashauri wananchi wenzangu tuwe kiini cha mabadiliko. Tufuatilie, tuulize maswali na tusimamie kwa makini utekelezaji wa MMES.

Haiingii akilini kuona kwa mfano wasichana waliohitimu elimu ya msingi wanaishia kufanyishwa kazi za nyumbani ama kuozwa wakiwa na umri mdogo kwa kisingizio cha kukosa shule.

Wanafunzi MEMKWA wapewe mahitaji muhimu

Richard Mkwiche, SLP 72762, Dar es Salaam

Tulipokea kwa furaha uamuzi wa Serikali kutoa elimu ya msingi bure nchini. Matarajio yalikuwa kwamba watoto wengi wangepata elimu bora zaidi. Pamoja na jitihada za serikali, bado idadi kubwa ya watoto wanaostahili kwenda shule wako mitaani.

Kundi hili ni la watoto wanaotoka katika familia zisizo na uwezo na yatima. Wazazi wa watoto hao hawana uwezo wa kununua sare na vifaa vya shule kwa watoto wao.

Kundi lingine ni la watoto wanaostahili kuandikishwa kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Watoto hawa ni wenye umri mkubwa au watu wazima, ambao baadhi yao wameoa. Wanaona aibu kusoma elimu ya msingi wanapojilinganisha na watoto wadogo walio katika shule za msingi za kawaida. Wengine wamefikia hatua ya kuacha masomo ili kukwepa fedheha waliyoipata.

Japokuwa umri ni tatizo, pia kukosa mahitaji kumesababisha idadi ya wanafunzi chini ya MEMKWA kuwa wachache. Idadi kubwa ya watoto hao wanaendelea kukosa elimu. Pamoja na nia njema iliyopo ya kuwapatia elimu, pia wanahitaji uhakika wa kupata chakula na sare. Kwa hali ya kawaida ni vigumu kwao kukaa darasani kusoma huku wakiendelea kukosa mahitaji muhimu kwa maisha yao.

Wizara ya Elimu na Utamaduni ifikirie uwezekano wa kutoa elimu ya msingi kwa walioikosa kwa njia ya posta na kuwasaidia kupata mahitaji ya msingi wale wanaokwenda darasani.

Ukurasa wa 2